

# Wanafunzi, wahadhiri Chuo Kikuu Mtakatifu Joseph waunda setilaiti

Na Mwandishi Wetu

**W**ANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph cha mkoani Dar es Salaam, kwa kushirikiana na wahadhiri wao wameunda setilaiti ambayo hadi kukamilika kwake itagharimu Dola za Marekani 250,000.

Wanafunzi hao ni Steven Makunga, David Seng'enge na Doris Ndaki wanaosoma Shahada ya Sayansi ya Kompyuta mwaka wa pili wakisaidiwa na mwalimu wao, Dk Amani Bura.

Utengenezaji wa setilaiti hiyo umefikia asilimia 50 na inatarajiwa kurushwa angani kuanzia mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka 2024 kutoa taarifa mbalimbali.

Akizungumza na HabariLEO jana, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Eliab Opiyo alisema mradi huo wa satilaiti unatekelezwa na wanafunzi na wahadhiri wa Kitivo cha Uhandisi na Teknolojia chuoni hapo.

Alisema wanatarajia kuipeleka setilaiti hiyo aina ya 3U Cubesat Kilometa 400 angani kuwezesha

ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya utafiti kwenye maeneo mbalimbali kama vile mabadiliko ya tabianchi na mienendo ya wanyamapori.

Profesa Eliab alisema walianzisha mradi huo miaka miwili iliyopita na kwamba kazi inayofanyika kwa sasa ni kutengeneza mfano wa setilaiti na kuifanyia majaribio kadhaa na kuongeza kuwa walishaionesha kwenye Maonesho ya Makisatu mkoani Dodoma.

Alisema watakapoirusha angani itawasaidia kupata taarifa kwa taasisi na watafiti wanaotafuta taarifa

mbalimbali.

Alisema kwa sasa mradi huo unafadhiliwa na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph ambacho kimekuwa kikigharimia ununuzi wa vifaa na kwamba mazungumzo ya kushirikisha watafiti na watu wengine bado yanaendelea.

Alisema mazungumzo hayo ni kwa ajili ya kushirikisha watafiti wa vyyuo na taasisi za kitafiti za kigeni kusaidia kutoa utaalamu na mafunzo zaidi ya kiufundi, vifaa vya setilaiti na huduma ya kuirusha setilaiti hiyo angani.

Steven Makunga ambaye ni mmoja wa wavumbuzi wa setilaiti hiyo, alisema wamefikia asilimia 50 ya kazi ya kuunda setilaiti hiyo na tayari inaweza kutumika kukusanya baadhi ya taarifa.

Alisema chombo hicho kitakuwa msaada mkubwa kwenye kupata taarifa za hali ya hewa na kwenye mawasiliano katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma hiyo.

Makunga alisema itasaidia pia kutoa taarifa za kilimo kwa wakulima kuhusu mazao ya kupanda na maendeleo ya mazao yao kwa ujumla.

## TAA yaomba kutotupa taka ngumu za plastiki Ziwa Victoria

Na Alexander Sanga, Mwanza

**M**AMLAKA ya Vianja vya Ndege Tanzania (TAA) imewaomba wakazi wanaoishi maeneo ya pembezoni



Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Dafroza Manyanda (wa ppe kushoto) akikahidhi vifaa vya usefi kwa...

## Hospitali ya Tunduru yatafuta wenye TB walioacha matibabu

Na Muhidin Amri, Tunduru

**H**OSPITALI ya Wilaya Tunduru mkoani Ruvuma kupitia kiten-go cha Kifua Kikuu na Ukoma inawatafuta waliobainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa Kifua Kikuu (TB) ambao wameacha kuendelea na matibabu na hawajulikani walipo.

Msako huo unawahusisha wataalamu wa kitengo cha kifua kikuu na...